JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

# TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI MACHI NA APRILI, 2024

## 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha miezi ya Machi na Aprili, 2024 vipindi vya mvua viliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, maeneo mengi yalipata mvua za juu ya wastani hadi wastani ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa miezi ya Machi na Aprili. Vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo. Hali hii ilisababisha mafuriko, uharibifu wa miundombinu na mali pamoja na vifo. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika maeneo machache ya ukanda wa Pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa mvua za Maika, 2024 na Msimu, 2023/2024.


### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Machi, 2024

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2024 vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo vilijitokeza katika maeneo mengi nchini. Aidha, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua za juu ya wastani hadi wastani ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa mwezi Machi. Vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha mafuriko, uharibifu wa miundombinu na mali, kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi pamoja na vifo.  Mnamo tarehe 22 Machi, 2024 kituo cha Moshi (mkoa wa Kilimanjaro) kilipima milimita 108.2 za mvua kwa saa 24 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kwa mwezi Machi, 2024 ikifuatiwa kituo cha Tumbi (mkoa wa Tabora) kilichopima milimita 97.6 na Mahenge (Mkoa wa Morogoro) milimita 93.3 mnamo tarehe 31 Machi, 2024.

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2024 ukanda wa pwani ulipata vipindi vingi vya mvua kubwa. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ndani ya saa 24 ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 1.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz




**Kielelezo 1:** Vituo vilivyoripoti viwango vya mvua kubwa kiasi cha milimita 50 au zaidi ndani ya saa 24 kwa mwezi Machi, 2024.

Taarifa kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari zilithibitisha kutokea kwa athari katika baadhi ya mikoa ikiwemo mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro, Lindi na Mtwara baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko, uharibifu wa mali na kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi.



**Kielelezo 2**. Wananchi wakipitia kwenye barabara iliyofurika maji Kilosa, Morogoro (Chanzo: *Millard Ayo*).

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*

**1.2 Hali joto kwa mwezi Machi, 2024**

Katika kipindi cha mwezi Machi 2024, hali ya joto iliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, hali ya joto zaidi ilijitokeza katika maeneo machache, hususan yale yaliyopo mwambao wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 36.0°C kilirekodiwa katika kituo cha JNIA (Dar es Salaam) mnamo tarehe 3 Machi 2024 kikifuatiwa na nyuzi 35.7 °C na 35.5 °C vilivyorekodiwa katika kituo cha JNIA (Dar es Salaam) na Kibaha mnamo tarehe 08 na 10 Machi, 2024 mtawalia. Aidha, Vituo vya Zanzibar na Moshi viliripoti nyuzi joto 35.4 °C na 35.0 °C mnamo tarehe 11 na 12 Machi, 2024.

**1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Machi, 2024**

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2024 vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika maeneo machache ikiwemo ukanda wa pwani (Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba). Nguvu ya upepo ilisababisha athari mbalimbali ikiwemo kusambaa kwa vumbi, kupeperushwa kwa takataka na kusababisha kupungua kwa uono. Maeneo machache ya mwambao wa pwani ya bahari yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika maeneo ya mwambao.


**1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Aprili, 2024**

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2024 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, vipindi vichache vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo mbalimbali. Mnamo tarehe 13 Aprili, 2024 kituo cha Lyamungu kilichopo mkoani Kilimanjaro kilipima milimita 179.1 za mvua kwa saa 24 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kwa mwezi Aprili, 2024, ikifuatiwa na vituo vya Pemba na Moshi vilivyoripoti milimita 140 na 133.5 mnamo tarehe 18 na 13 Aprili, 2024 mtawalia. Jedwali 1 linaonyesha idadi ya siku ambazo vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi.

| Kanda | Kituo | Idadi ya siku | Mvua kubwa (mm) |
|---|---|---|---|
| **Pwani ya Kaskazini** | Zanzibar | 4 | ≥ 50 |
| | JNIA (Dar es Salaam) | 3 | ≥ 50 |
| | Kibaha | 2 | ≥ 50 |
| | Pemba | 4 | ≥ 50 |
| | Kizimbani | 3 | ≥ 50 |
| | Dar Port | 3 | ≥ 50 |
| **Nyanda za juu kaskazini mashariki** | Arusha | 2 | ≥ 50 |
| | Lyamungu | 8 | ≥ 50 |
| | Moshi | 2 | ≥ 50 |
| | Babati | 1 | ≥ 50 |
| **Ukanda wa Ziwa** | Bukoba | 1 | ≥ 50 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Victoria** | Ukiriguru | 2 | ≥ 50 |
| | Mwanza Marine | 1 | ≥ 50 |
| **Kati** | Singida | 1 | ≥ 50 |
| **Magharibi** | Mpanda | 1 | ≥ 50 |
| | Tumbi | 1 | ≥ 50 |
| **Nyanda za juu kusini magharibi** | Sumbawanga | 1 | ≥ 50 |
| | Mahenge | 2 | ≥ 50 |
| **Pwani ya Kusini** | Kilwa | 1 | ≥ 50 |
| | Mtwara | 1 | ≥ 50 |

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2024 ukanda wa pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki ulipata vipindi vingi vya mvua kubwa. Kituo cha Lyamungu kilichopo Kilimanjaro kilipata vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ndani ya saa 24 kwa siku nane. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 70 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 3.




**Kielelezo 3:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Aprili, 2024

Taarifa kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari zilithibitisha kutokea kwa athari katika baadhi ya mikoa ikiwemo mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro, Arusha na Kilimanjaro baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko, uharibifu wa mali na kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi na vifo.



**Kielelezo 4:** Nyumba zikiwa zimezingirwa na maji baada ya mvua kubwa Karatu, Arusha (*Chanzo:Gazeti Mwananchi*).

**1.5 Hali joto kwa mwezi Aprili, 2024**

Katika kipindi cha mwezi Aprili 2024, hali ya joto ilijitokeza katika maeneo machache, hususan ukanda wa pwani. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 34.1 °C kilirikodiwa katika kituo cha Tanga mnamo tarehe 12 Aprili, 2024. Aidha, katika kipindi cha mwezi Aprili, 2024 hakukuwa na vipindi vya joto kali sana vilivyorekodiwa.

**1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Aprili, 2024**

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2024 vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba), hususan nusu ya pili ya mwezi. Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 10 Mei, 2024*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**